

Maddili Msingi na Kanuni za Kuongoza

Imani Ya Msingi

Sisi sote tunazingatia tamko la Imani la Mama waombaji wa kimataifa, mtu binafsi kumkubali Yesu kwenye maisha yake kama Bwana na Mwokozi na kwamba Yesu ni Mungu.

Tunaamini kuwa kupitia maombi Mungu huachilia nguvu zake kwa watoto wetu na shule. Imani yetu iko kwa Mungu anayesikia na kujibu maombi yetu.

Kusudi la msingi

Tamko la Utume: Mama waombaji wa kimataifa hugusa Watoto na shule ulimwenguni kwa ajili ya Kristo wanapokusanyika mama kuomba

Maono: Maono yetu ni kila shule ulimwenguni kufunikwa na maombi.

Vipaumbele vya msingi

- Mungu Kwanza
- Familia ya Pili
- Huduma ya Tatu

Muundo na Njia kuu

- Kuomba kwa kunia mamoja
- Hatua Nne za Maombi
- Kuomba kwa kutumia Maandiko
- Kuomba kwa kuzingatia
- Kuomba Uinjilisti

Kanuni za Kutuongoza

Sisi ni watumishi waliouunganishwa na Bwana kumtegemea kabisa

Atuongoze na kutusaidia.

Hatutegemei magari au farasi, bali Jina la BWANA, Mungu wetu. Zaburi 20: 7

Sisi ni Wanafunzi na huduma inayoongezeka.

Uanafunzi: kuwafundisha wanawake jinsi ya kuomba na kumwamini Mungu

Kuongezeka: kwenye kila shule inayoombewa na kikundi

Tumeitwa kutumika kwenye huduma ya Mama waombaji.

Tunawajibika kuwakilisha huduma na maono kwa upendo na uadilifu.

Tunalea, tunatia moyo na kuandaa kwa roho ya uungu, yenye neema, isiyokosoa tukiwa mfano wa mwanamke wa kibiblia mwenye usafi wa kijinsia.

Tunaamini kwa dhati na kuunga mkono ndoa ya kibiblia iliyoanzishwa na Mungu kama agano la uhusiano katika ya mwanamume mmoja na mwanamke mmoja.

Tuna ujumbe unaoleta faraja na matumaini kwa akina mama.

Tunatunza siri kwa hali ya juu - tunachokiombea kwenye kikundi, kinabaki kwenye kikundi.

Tunawaombea watoto na shule.

Sisi **sio** kikundi cha kushawishi: *Mama waombaji wa kimataifa si kikundi cha kufanya ushawishi, hata uwe wenye thamani. Ushiriki kwenye mambo ya nje ya kisiasa na kijamii lazima yafanyike na mtu binafsi. Kwa namna yoyote ile jina la Mama waombaji wa kimataifa lisitumike kwenye mambo nje.*

Tutawasiliana na wadau wanaotusaidia kifedha kwa viwango vya juu vya taaluma na vyenye ukweli.